

Utenzi ufuatao umeandikwa na Mshairi Mwamede Semboja wa Oslo, Norway kwa jina la kishairi anajitambulisha kama “Kighono Mbeungwa” Shairi lake linazungumzia penzi.

PENDO LA KHAINI

1. Nimechoka nawe, uso na imani.
Ata nipumuwe, ewe kisirani.
Usinizuzuwe, nishakubaini.
Pendo la khaini, halidumu sana.

2. Nalipokupenda, na kukuthamini.
Ukafanya inda, kunionya kani.
Moyo meuvunda, pasi na amani.
Pendo la khaini, halidumu sana.

3. Tamati uliko, pulika lisani.
Nenda nitokako, niketi makini.
Langu sikitiko, litafiya ndani.
Pendo la khaini, halidumu sana.

*Mwamede J. W. Semboja (Kighono Mbeungwa)
Oslo, Norway
August, 2002*